# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - TAMISEMI
# SHULE YA SEKONDARI LUGEYE
# S.L.P 248 MAGU - MWANZA

Kumb. Na. LGSS/ADM/8
*Mawasiliano:-*
*Mkuu wa shule: 0758098727*
*Makamu Mkuu wa Shule: 0753751957*
*Mtaaluma: 0767160415*
*Matroni: 0622868889*

*Mzazi/mlezi wa* ..................……………………………………………

YAH: **<u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO ................</u>**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao …………………………….............................. amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha Tano katika shule hii. Tunampa hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano mwaka ...................... katika mchepuo/tahasusi ya ………….

Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **...............**, mwisho wa kuripoti ni tarehe **.........................**

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Lugeye iko mashariki mwa Jiji la Mwanza katika wilaya ya Magu kilomita 35 kutoka jijini Mwanza na kilomita 20 kutoka Magu mjini. Ukiwa Magu shule iko magharibi mwa mji wa Magu.

**1. JINSI YA KUFIKA SHULENI**

Ukifika Mwanza mjini, **nenda stendi ya mabasi Nyamhongolo**, hapo stendi panda mabasi yaendayo Magu, Bunda ama Musoma (panda Hiace ama Coaster/TATA) mwambie kondakta akushushe Lugeye. Ukishuka stendi ya Lugeye, elekea upande wa Magharibi kama mita 400 utakuwa umefika shuleni, shule ipo kandokando mwa barabara kuu ya Mwanza-Musoma na ina utambulisho wa kibao chake "sign post". Ukiwa unatokea Musoma, Bunda, Bariadi ama Magu, panda mabasi yaendayo Mwanza na shuka Lugeye stendi kisha nenda mbele kidogo kama unaelekea Mwanza kwa kufuata barabara ya lami kama mita 400 hivi utaona ubao wa shule mkono wako wa kushoto hapo ndipo shuleni Lugeye sekondari.

Kutoka Mwanza nauli Kwa Coaster/TATA/Hiace ni kati ya Tsh.2000/= na 1500/= na kwa mabasi makubwa nauli ni Tsh.2000/= ama 3000/=. Kutoka Magu mjini nauli ni Tsh.1000/= tu.
Shule itafunguliwa tarehe ___________ na masomo kwa kidato cha tano yataanza tarehe _________ fika shuleni tarehe __________, **ukiwa na barua hii ya wito**. Kama hutapenda kujiunga na shule hii toa taarifa mapema kabla ya shule kufunguliwa. Hakuna sababu itakayokubalika kwa mwanafunzi yeyote kutofika shuleni mapema. Hali kadhalika jiepushe na aibu ya kuumbuka kwa kuja shuleni na jina la mtu mwingine.

## MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

**A. MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhali | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |
| | **Aje na Bima ya Afya, kama hana bima ya afya aje na Tsh. 50,400/=** kwa ajili ya kumkatia bima | |

**Maelezo muhimu:-**

Mwanafunzi afike shuleni akiwa na;

Bank pay slip, Malipo yote yalipwe katika Akaunti ya LUGEYE SEC. SCHOOL RECURRENT ACCOUNT namba **31201200082** Bank ya **NMB**

**NB. Hatupokei pesa taslimu hapa shuleni, isipokuwa fedha kwa ajili ya kumkatia bima ya afya aje nayo shuleni**

**B. SARE YA SHULE NA MAVAZI MENGINE**

**1. SARE**

i. Sketi 2 za darasani zenye rangi ya damu ya mzee. Sketi hii iwe na rinda box( inch 8 hadi 9) upande wa mbele na nyuma wa sketi, sketi iwe na urefu kufika kwenye kifundo cha mguu (ankle), iwe na mfuko mmoja mkono wa kulia na zipu iwe pembeni mkono wa kushoto, isiwe inabana na iwe na belt.Pembeni iwe na marinda madogo matatu pande zote mbili.

ii. Mashati 2 meupe aina ya tomato ya mikono mirefu yasiyobana

NB. Kwa waislam, sare ni sketi ndefu yenye rangi ya damu ya mzee, mashono, mtindo na idadi ni kama ilivyoelekezwa hapo juu (i).

Shati ni half kanzu (nusu kanzu) mikono mirefu kitambaa aina ya halua pamoja na juba jeupe linalofunika mikono, kitambaa aina ya halua. Idadi kama ilivyoelekezwa hapo juu (ii)

**2. NGUO ZAKUSHINDIA**

Gauni 2 za kushindia, aina ya kitambaa **kunguru damu ya mzee grade one**, yawe na urefu unaofikia kifundo cha mguu na yasiwe yanabana, yawe na mikanda na kola kwa mbele. Kwa muislam atavaa gauni pamoja na juba aina ya kitambaa tetron damu ya mzee.

**3. NGUO ZA MICHEZO**

Suruali 1(tracksuit) rangi nyeusi yenye lastiki kwa ajili ya mazoezi na michezo

Zingatia kununua Track suit kubwa inayotosha vizuri binti yako. Akija na track suit inayombana hataruhusiwa kuivaa.

**4. MATANDIKO**

Shuka 2 za pinki iliyokolea pamoja na foronya 1 ya pinki iliyokolea pamoja na mashuka mawili mengine rangi ya light blue pamoja na foronya moja (01) ya light blue.

**5. MAVAZI MENGINE AMBAYO PIA NI SARE YA SHULE**

i. Tai 1 rangi ya damu ya mzee

ii. T-shirt ya rangi ya blue yenye kola na nembo (ukipenda inapatikana shuleni 13,500/=)

iii. Sweta la blue lenye nembo (ukipenda linapatikana shuleni 13,500/=)

**6. VITU VINGINE NI PAMOJA NA**

i. Viatu vyeusi vyenye kamba vya ngozi (siyo buti) jozi mbili ii. Soksi nyeupe aina ya stockings pea mbili iii. Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo iv. Chandalua 1 cha 4ft x 6ft cheupe v. Blanket 1 ni hiari vi. Taulo 1, khanga au vitenge jozi moja

**Vifaa vya usafi**

-Ndoo mbili za plastiki lita 20 kila moja na beseni moja la kufulia

- PCB – Mfagio 1 wenye mpira wa kudekia (squeezer) na fagio moja laini la kufagilia (soft bloom)

- CBG – Blash ngumu ya kusugulia sakafu (hard bloom) na blash ngum fupi ya kusugulia masink ya vyoo.
- HGK – Fagio laini la kufagilia (soft bloom) na Blash ngumu ya kusugulia sakafu (hard bloom)
- HGL – Fagio laini la kudekia na ndoo yake (mopper).
- HKL – Fagio laini la kufagilia (soft bloom) na fagio moja yenye mpira wa kudekia (squeezer)
- HGFa –Jembe na mpini wake pamoja na kotama moja (01)
- HGLi –Jembe na mpini wake pamoja na kotama moja (01)

**NB:** Vifaa vyote vilivyoorodheshwa hapo juu vinapatikana karibu na mazingira ya shule

viii. **Vifaa vya taaluma**

- Ream paper 2 yaani:

  (i). Double A moja (1) - kwa ajili ya kuchapishia mitihani

  (ii). Ream paper moja (1) aina ya A4 (Yenye uzito wa karatasi 80gm) kwa ajili ya mazoezi na mitihani, hivyo **kwa mwaka** jumla rimu mbili. Ziletwe muhula wa kwanza siku ya kuripoti shuleni.
- Daftari kaunta quire 4 kuanzia saba na kuendelea
- HKL na HGL wanashauriwa waje na oxford advanced leaners dictionary (10 edition au 11 edition
- HGK na HKL wanashauriwa waje na kamusi ya kiswahili ya TUKI (Toleo la 4)

- Kwa wale wa PCB na CBG waje na dissecting tray, Non- programmable scientific calculator, na stop watch.
- Taa ya sola/tochi kwa ajili ya kujisomea pindi umeme ukikatika
- Kalamu za wino na kalamu za mkaa ( penseli) za kutosha
- Mwanafunzi anashauri kuja na Vitabu vya masomo ya tahasusi kwa kila somo la tahasusi yake (Orodha imeambatanishwa)

**C. <u>MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI</u>**

(i). Chombo cha kuhifadhia maji safi ya kunywa cha lita 5

(ii). Vifaa vya usafi binafsi kama pedi za kutosha, mswaki, kiwi, brashi ya viatu vyeusi, dawa ya meno, sabuni, losheni, mafuta ya kujipaka, kitana, toilet paper, n.k.

(iii). Vifaa vya kulia chakula ambavyo ni bakuli, sahani,kikombe, kijiko nk

(iv). Afike na mashuka ya kutosha ya kujifunika, mto 1 na godoro 1 la 3”x 6”

(v). Nguo za ndani za kutosha kama vile shimizi/gagulo, chupi, night dress, skin tight

## D. MAAGIZO MENGINE

1. **Fedha za matumizi:** Mwanafunzi haruhusiwi kwenda mjini. Mzazi ahakikishe anamnunulia binti yake mahitaji muhimu, pia ampe fedha ya kutosha kwa ajili ya matumizi madogomadogo ambayo hupatikana katika duka lililopo hapa shuleni. Endapo mzazi atalazimika kumtumia binti yake pesa zaidi awasiliane na Mkuu wa shule kwa namba **075098727** ama Makamu Mkuu wa shule kwa namba **0753751957** ili apewe utaratibu wa jinsi gani anaweza akatuma pesa hiyo.
2. **Nauli:** Sharti mtoto apewe nauli ya kumrudisha nyumbani kila mwisho wa muhula. Hatuna huduma ya chakula, malazi wala masomo wakati shule zinapofungwa katika likizo kubwa. Mzazi asiyempa binti yake nauli na fedha ya matumizi shuleni huku ni kumnyima haki yake ya msingi ya upendo. Hata hivyo wanafunzi wanaruhusiwa kubaki shuleni wakati wa likizo fupi ya mwezi Machi na Septemba. Mzazi atoe idhini endapo atamruhusu binti yake kuondoka shuleni wakati wa likizo hiyo fupi kwenda kwa ndugu anayeaminika na familia.
3. **Msamaha wa ada:** Suala la ada na mahitaji muhimu ya mtoto anayetoka katika mazingira magumu lishughulikiwe kikamilifu na mzazi au mlezi wake. Shuleni hakupatikani msamaha wala huduma maalumu kwa watoto/wanafunzi wa aina hiyo. Wanafunzi wote ni sawa, wanapata huduma na haki sawa shuleni. Hivyo ana wajibu wa kutoa malipo yote kwa huduma zote za kishule bila kujitenga.
4. **Vyeti bandia vya hospitali na matibabu:** baadhi ya wazazi hushirikiana na mabinti zao kutafuta vyeti bandia ili mabinti zao wasifanye kazi za shule, mzazi atoe taarifa mapema juu ya maradhi sugu au mazingira magumu anayokuwa nayo mtoto/mwanafunzi hata hivyo mtoto/mwanafunzi atafanya kazi kama wenzake wote anapokuwa hajakabiliwa na tatizo au tatizo sugu la ugonjwa atakaokuwa nalo.
5. **Kujaza fomu:** Siku ya kuwasili shuleni kwa mara ya kwanza, mwanafunzi anatakiwa kuleta barua hii, pamoja na fomu zilizotajwa hapo chini zikiwa zimejazwa kikamilifu taarifa zake zote zinazotakiwa.

## VIAMBATANISHO

A. Historia ya mwanafunzi

B. Medical examination form

C. Ndugu watakaomtembelea mwanafunzi

D. Kiapo cha mwanafunzi E. Kiapo cha mzazi

**Kiambatanisho B;** fomu hii ijazwe kikamilifu na kugongwa muhuri na daktari wa hospitali ya serikali ya Wilaya, Mkoa au Rufaa. Ni lazima mzazi ahakikishe kuwa binti yake anapimwa kweli. Taarifa ya Mganga atakayejaza fomu hii itakuwa ni kielelezo pekee kitakachochukuliwa shuleni kuhusiana na afya ya binti yako. Sharti apimwe kwa makini na ijazwe kikamilifu. Hatupokei taarifa ya afya toka Hospitali isiyokuwa ya serikali. **ANGALIZO:** Mzazi/mlezi ahakikishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na sahihi ya mganga tu. Mwanafunzi atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukuliwa vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.

**Kiambatanisho C;** Historia kamili ya mwanafunzi na maelezo yake binafsi yajazwe na mzazi/mlezi kwa ufasaha kwa ajili ya kumbukumbu za shule

**Kiambatanisho D;** Mzazi/ Mlezi aorodheshe ndugu wa karibu hapa mkoani Mwanza watakaomwona mwanafunzi siku ya "visiting day" na pia atakaokwenda kuwaona yeye ama shule kufanya nao mawasiliano kwa niaba ya mzazi/mlezi panapokuwa na uhitaji huo.

**Kiambatanisho E**; Hali kadhalika ahadi ya kutii sheria, amri na mamlaka ya shule ijazwe kikamilifu.

Mwanafunzi pia aje na nakala ya hati ya matokeo kidato cha nne, nakala ya cheti cha kuzaliwa (Photocopy of birth certificate) au cheti cha uraia endapo mwanafunzi siyo raia wa nchi hii.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (Wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulusha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI / MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VYEMA UKAWASILIANA NA**

**UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- **Mkuu wa shule:** ***0758098727***, 
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0753751957** , 
- **Matroni: 0622868889**

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA SAFARI NJEMA KARIB[illegible]IA
LUGEYE SEKONDARI

HEADMISTRESS
LUGEYE SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 248
MAGU

**ANGELA E. RUBILYA**
**MKUU WA SHULE 07580987**

## SHERIA ZA SHULE

A. **MASOMO**

Kila mwanafunzi lazima aelewe lengo la Taifa kwa yeye kuwepo hapa kuwa ni kumpa elimu atakayoitumia baadae kwa manufaa yake binafsi na umma kwa ujumla. Hivyo sharti mwanafunzi:-

1. Awahi mahali popote anapotakiwa. Hii ni pamoja na kurudi shuleni siku anayotakiwa kila mwanzo wa muhula na likizo za katikati ya muhula.
2. Ahudhurie masomo yote ya darasani. Ifahamike kwamba shughuli za shamba, michezo na usafi ni shughuli za kielimu. Mwanafunzi afanye kazi zote za masomo na za nje ya darasa na kuziwasilisha kwa mwalimu kwa wakati unaotakiwa bila visingizio kwa kiwango kinachotakiwa.
3. Ni marufuku kupiga kelele, kuandika barua na kupiga gumzo wakati wa masomo au maandalio (prep) za alasiri na usiku. Sheria za maktaba ziheshimiwe na za maabara. Pia mwanafunzi asizurure nje wakati wa masomo na atumie vema mda wake.
4. Ni marufuku kuingia kwenye maabara, chumba cha waalimu, Ofisi za shule, stoo au jikoni bila mwalimu kuwepo au kupewa kibali na mwalimu.

B. **MAVAZI**

1. Mwanafunzi atavaa vazi rasmi la Shule wakati wa masomo, safari, aendapo mjini na awapo nje katika shughuli zozote za kishule. Vazi la kushindia au la michezo ni marufuku kuvaliwa darasani wakati wa vipindi.
2. Makoti, mizura, vilemba, bangili, heleni, mikufu, Pete, rozali/tasbihi, vidani, vipuli na mapambo yoyote hayaruhusiwi kuvaliwa pamoja na vazi rasmi la Shule wala vazi la kushindia.
3. Mwanafunzi awe na nywele fupi wakati wote haruhusiwi kusuka wala kutia dawa. Mwanafunzi awe nadhifu daima na apendeze bila kujiremba, kujipodoa au kujipamba.
4. Mavazi yote (binafsi au ya shule) Atakayovaa mwanafunzi akiwa ndani au nje ya mipaka ya shule ni lazima yawe ya heshima.

**MUHIMU:** Mavazi ya nyumbani kama nguo, viatu, mapambo, n.k hayaruhusiwi kabisa shuleni.

C. **RUHUSA**.

1. Mwanafunzi hataruhusiwa kusafiri au kulala nje ya shule wakati wote wa kipindi cha masomo. Shughuli za kidini na za Kifamilia zitakazolazimu wanafunzi walale nje ya shule zipangwe wakati wa likizo kwani wanafunzi hawaruhusiwi kushiriki wakati wakiwa kwenye masomo.
2. Mtoto hataruhusiwa kwenda kwa ndugu, ofisi za mabasi kama Bunda bus, Bank au Posta kufuatilia ujumbe, pesa, barua, mizigo au vifurushi. Wazazi watume ofisi za posta na simu kuepusha usumbufu huu kwa wanafunzi.
3. Mwanafunzi ataruhusiwa na mkuu wa shule kuhudhuria msiba kama aliyefariki ni baba, mama, mlezi, kaka au dada wa tumbo moja. Ruhusa haitolewi kwa ndugu wengine hata kama msiba huo umetokea nyumbani kwa mwanafunzi huyo.
4. Ni marufuku mwanafunzi kwenda nyumba za walimu ama nyumba ya matron isipokuwa patokeapo shida isiyoweza kuzuilika na apate idhini kwa mwalimu wa zamu.

**D. CHAKULA:**

1. Ni marufuku kubebeana chakula. Wagonjwa waliolazwa zahanati watapelekewa chakula na wale wanaohusika tu. Ni marufuku kupeleka chakula mabwenini au madarasani.
2. Ni lazima kuwapo na kuwahi saa za chakula daima na ni marufuku kupiga kelele wakati chakula, usafi binafsi, unadhifu na utulivu uzingatiwe.
3. Ni marufuku kutupa hovyo takataka kama mabaki ya chakula, maganda, karatasi n.k Takataka zitupwe kwenye vyombo na mashimo ya takataka yaliyotengwa kwa kazi hiyo.
4. Wenye zamu za usafi wa eneo la kugawa chakula wahakikishe hali ya usafi kila baada ya chakula. E.

E. **AFYA.**

1. "MLINZI MKUU WA AFYA YAKO NI WEWE MWENYEWE". Kila mwanzo wa muhula uhakikishe umepimwa na daktari na kupata matibabu yanayostahili kujihakikishia afya njema daima uwapo shuleni.
2. Daktari na mzazi ni lazima kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ikiwa mtoto ana maradhi ya kurithi au kudumu kama pumu, moyo, sickle cell n.k. Mtoto kama huyu alete akiba ya kutosha ya madawa yake kwa sababu shule haina madawa ya maradhi kama hayo.
3. Mwanafunzi akiugua akiwa Shuleni atoe taarifa kwa mwalimu wa zamu na atapata huduma katika zahanati. Ikibidi atapelekwa Hospitali kwa uchunguzi na huduma zaidi. Ikishindikana atarudishwa nyumbani mara moja.
4. Ni jukumu la Mkuu wa Shule kutoa taarifa kwa mzazi endapo mwanafunzi atazidiwa. Taarifa zitakazowafikia wazazi kwa njia nyingine yoyote ni batili.
5. Matumizi sahihi ya vyoo yazingatiwe. Adhabu kali itatolewa kwa atakayebainika akitumia vyoo vibaya, au kukwepa kufanya usafi wa vyoo.

F. **KUSALI.**

Wanafunzi wote watasali kwenye madhehebu yao hapa Shuleni. Ikiwa sherehe au tukio pekee la kidini litawakuta watoto Shuleni huenda wakaruhusiwa kwenda kusali nje ya shule kwa kibali maalumu cha Mkuu wa Shule. Wanafunzi watavaa vazi rasmi la shule katika shughuli hiyo. Atakayekwenda kinyume na ruhusa hii atashughulikiwa kikamilifu chini ya kifungu cha taratibu atakazokuwa amekiuka.

G. **SIMU**

***Nimarufuku mwanafunzi kumiliki simu shuleni au darasani. Aidha wanafunzi wataruhusiwa kuwapigia wazazi tu kila mwisho wa mwezi kupitia namba ya Matroni. Haruhusiwi mwanafunzi kutumia simu na namba mbalimbali za watumishi kwa ajili ya mawasiliano binafsi. Mzazi unaruhusiwa kupiga simu kwenye namba ziliwekwa kwenye fomu hii ya kujiunga na shule tu.***

H. **<u>MAKOSA YANAYOMSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.</u>**

1)Uasherati (2) Utoro (3) Kudharau Bendera, Wimbo au fedha za Taifa (4) Kupigana (5)Kuharibu kwa makusudi mali ya umma (6)Ulevi wa aina yoyote (7) Kutumia au kuwa na madawa ya kulevya (8)Kujihusisha na mambo ya kishirikina (9) Matusi kwa walezi hapa shuleni, viranja, wanafunzi wenzake au kwa yeyote yule (10)Wizi (11)Kupata mimba (12)Kutoa mimba (13) Kulala nje ya shule (14)Makosa yenye kujirudiarudia (15) Kukataa kufanya adhabu (16)Kuongoza migomo au fujo yeyote shuleni (17) Kuvuruga Amani ya jamii ya shule (18) Kupeleka mgeni bwenini (19) Makosa ya jinai.

**<u>NYONGEZA NA 1. YA SHERIA ZA SHULE</u>**

Ni marufuku kwa wanafunzi kuwa na vitu vya thamani kwa matumizi binafsi kama vile:

i. Majiko na vifaa vingine vya kuchemshia maji au kupikia ii. Simu za aina yoyote iii. Radio na vifaa vinginevyo vya muziki za aina yoyote iii. Radio na vifaa vinginevyo vya muziki iv. Kompyuta na viambata vyake v. Runinga deki na vinginevyo vi. Kamera za video na za kawaida vii. Radio za mfukoni, radio call n.k viii. Dhahabu na vitu vinginevyo vya thamani na nguo za nyumbani

**ATAKAYESEMEKANA AU KUKAMATWA NA KITU CHOCHOTE KATI YA HIVYO ATAADHIBIWA VIKALI, ATANYANG'ANYWA VIFAA HIVYO NA VITAKUWA NI MALI YA SHULE.**

**<u>NYONGEZA NA 2 YA SHERIA ZA SHULE.</u>**

Ni marufuku na ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kujenga mazoea na mahusiano binafsi na Mwalimu, watumishi wengine na/au wanafamilia zao. Wazazi wanaruhusiwa kumwona/kuwasiliana na mkuu wa shule kutoa ujumbe muhimu wa haraka kwa mabinti zao kama kuna dharura kupitia namba za simu zitakazotajwa hapo awali. Sheria hizi zote zimewekwa kwa manufaa ya kuhakikisha kila mmoja anatenda na kutendewa haki. Sheria hizi hazina maana ya kumnyanyasa mtu yeyote ndani au nje ya shule hii.

**NAKUTAKIA KILA LA KHERI KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA NA TARATIBU ZOTE ZA SHULE.**

**KARIBU SANA**

**HALMASHAURI YA WILAYA MAGU**
**SHULE YA SEKONDARI LUGEYE**
**S.L.P 248, MAGU**

Bandika picha Moja ya Mwanafunzi Awe na shati jeupe

**KIAMBATANISHO A**
**HISTORIA NA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. MAELEZO BINASFI

Jina la mwanafunzi ……………………………………….

Majina ya wazazi

(i). Baba……………………………………………………………(hai/amefariki)

(ii). Mama…………………………………………….............................. (hai/amefariki)

Wazazi/Mzazi/Mlezi anakoishi…………………… Kabila la mwanafunzi ……………… Dhehebu la dini yake ………….......Tarehe ya kuzaliwa ……….......... wilaya alikozaliwa ……………. uraia nchi ya ……………… Jina la mlezi (kama anaishi na mlezi) …………………………………………
Uhusiano na mlezi ……………………………… Kazi ya Mzazi/Mlezi ………………………
Sehemu/Ofisi anayofanyia kazi mzazi/Mlezi………………………………………………………

Idadi ya ndugu katika familia (i)Wa kike…….(ii)Wa kiume…….. (iii) Wategemezi………... wangapi kuzaliwa katika familia………Afya yake kwa ujumla………………………… Matatizo maalumu aliyonayo mwanafunzi kitabia na kiafya ……........................................................

Uwezo/kipaji maalumu alivyonavyo mwanafunzi ……………………………………….

**2. SHULE ALIZOSOMA**

| SHULE | WILAYA/NCHI | MADARASA | MIAKA |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |
| 6. | | | |

**3.** MAELEZO YA NYONGEZA KAMA YAPO…………………………………………….............

**MAGU DISTRICT COUNCIL**
**LUGEYE SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 248**
**MAGU**

**<u>KIAMBATANISHO B</u>**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION (To be completed by Medical officer in respect to all form of entrants)**

Student's full name …………………………………………….. Age (Years) ………………. Blood count (red and white) ………………………………………………………… Stool examination …………………………………………………………………………

Urine analysis ………………………………………………………………………..

Syphilis and other venereal diseases test ……………………………………………….

T.B Test …………………………………………………………………………... Eye Test ……………………………………………………………………………...

Ears ………………………………………………………………………………

Chest Examination ……………………………………………………………..

Spleen ………………………………………………………………………….

Abdomen …………………………………………………………………………. Test for pregnancy ……………………………………………………………………..

Urine for plant test ……………………………………………………………………..

ANY ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical defect, chronic or Family diseases etc

…………………………………………………………………………………

I certify that the person named above is fit/unfit to pursue further studies in advanced level

Station ……………………………Signature …………………………………..

Designation …………………………………………………

Date ……………………………………………………………………………..

- ❖ Delete where necessary:

## HALMASHAURI YA WILAYA MAGU
### SHULE YA SEKONDARI LUGEYE
### S.L.P 248 MAGU

**<u>KIAMBATANISHO C.</u>**

**NDUGU WATAKAOMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI**

Mzazi/Mlezi wa …………………………………………………......kidato cha………20…

Utaratibu wa shule unawaruhusu wazazi/walezi wake na pia ndugu wengine wasiozidi watatu utakaowachagua wewe mwenyewe kufika shuleni kumjulia hali binti yako. Wageni hawa wataruhusiwa kuonana na mwanafunzi. Wageni hupokelewa na mwalimu wa zamu ili kupokea maelekezo na salamu za mzazi/mlezi ama ndugu na kumfikishia mwanafunzi hata hivyo wageni hawaruhusiwi shuleni miezi ya Oktoba, Novemba na Mei kwa sababu ya kuwepo mitihani ya taifa hapa shuleni. Tafadhali tuorodheshee ndugu wa karibu walioko Mkoa wa Mwanza ambao ungependa wafike kumjulia hali binti yako. Kwa siku za kazi ni vema wageni wafike saa za masomo kuweza kupata fursa ya kuonana na mwalimu wa darasa la mtoto ili kujua maendeleo yake kitaaluma pia.

| **TAARIFA** | (1) | (2) | (3) |
|---|---|---|---|
| 1.Jina la ndugu | | | |
| 2.Kazi yake | | | |
| 3.Uhusiano naye | | | |
| 4.Anakoishi | | | |
| 5.Anuani yake | | | |
| 6.Simu yake | | | |
| 7.Picha (Pasport size) | | | |

**8.** Nimeelewa maelezo hayo hapo juu. Nina maoni yafuatayo (Eleza kama yapo)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

Saini ya Mzazi/Mlezi………………………………Tarehe…………Saini ya Mwanafunzi……………………..…Tarehe…………………………………

Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………

**HALMASHAURI YA WILAYA MAGU**
**SHULE YA SEKONDARI LUGEYE**
**S.L.P 248 MAGU**

**VIAMBATANISHO D**

**AHADI YA KISHERIA AMRI NA MAMLAKA YA SHULE**

3. Mimi (Mwanafunzi)…………………………………………………………nimesoma kwa makini sheria zote za shule na nyongeza Na 1 na Na 2 ya sheria za shule, Nimezielewa barabara na nakubali kwa hiari yangu kuzitii na kuziheshimu. Nitafanya kazi na kusoma kwa bidii ili kijijengea msingi bora wa maisha yangu ya baadaye ili kujiletea heshima na sifa yangu binafsi kwa ujumla.

   Ndimi mwanafunzi

   (jina)……………………………………………………………….

   Saini………………………………………Tarehe…………………………………..

**KITAMBULISHO E.**

4. Mimi…………………………………………………….Mzazi/Mlezi nimesoma sheria na taratibu za Shule. Nimezielewa nami nakubali binti yangu ajiunge/asijiunge na masomo katika shule hii. Pia naahidi kulipa ada na michango yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo ya Shule. Nitahakikisha kukamilisha madai yote ya shule kabla ya mwisho wa kila mwaka wa masomo wa binti yangu kumuwezesha kuendelea na masomo bila bugudha yoyote.

Ndimi mzazi/Mlezi (jina)………………………………………………………………

Saini………………………………………….

Namba za simu za wazazi/walezi ............................................









**KITAMBULISHO F.**

**TAALUMA: -**

Kwa kuwa shule ina uhaba wa vitabu, inashauriwa mwanafunzi aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:-

**I. VITABU VYA CHEMIA**

1. Jain s.k (2006) *Conceptual Chemistry XI, 4th edition*. Chand, New delhi India
2. Ngaiza lusima (2014) *Atomic Structure and Bonding*. Hopegen company ltd. Dar es Salaam. Tanzania
3. Ngaiza lusima (2014*) Physical Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
4. Ngaiza lusima (2014) *Inorganic Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
5. Ngaiza lusima (2014) *Environmental and Soil Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania.
6. E. Ramsden (2001) *Calculations for A-level chemistry*.

**II. VITABU VYA BIOLOJIA: -**

1. .Gleen and Toole (1999). *Understanding Biology 4th Edition*.Stanlye Thomes LTD UK.
2. Kent M. (2013). *Advanced Biology*.Oxford University Press LTD 2nd Edition
3. Aggarwal S. (2017). *A text book of CBSE.Biology for Class XI*.Nijra Publishers and Printers PVT.LTD
4. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VI.*Chand and Company LTD.New Delh
5. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VII*.Chand and Company LTD.New Delh
6. Taylor etal (1997) *Biological Science.3rd Edition,* Cambridge University Press LTD.
7. T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Six,* Dar es salaam, T.I.E
8. T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Five,* Dar es salaam, T.I.E

## III. VITABU VYA HISTORY: -

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M. (2015) *Understanding African History*, Paper 1, New Version, Mikumi Publishers.

2. Kato, A.K. (2012) *Mastering Advanced Level History Book 1*, Mwanza, Mweas Book Publishers
3. Kato, A.K (2012) *Mastering Advanced Level History Book 2*, Mwanza, Mweas Book

   Publishers
4. Samwel, S & Stephen. O (2008) *World History Advanced Level*, Dar es salaam, Nyambari Nyangwine Publishers.

5. Shibitali, C.K (2017) *Contemporary Historical Events,* Third Edition, Dar es salaam, Che Guevara Investment.

6. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 1*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press.

7. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 2*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press .

8. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools Form Five*, Dar es Salaam, T.I.E.

9. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools,* Form Five, Dar es Salaam, T.I.E

## IV. VITABU VYA KISWAHILI: -

1. Masebo, J.A & Nyangwine. N (2010) *Tahakiki Kidato cha 5& 6.* Nyambari Nyangwine Publisher, Dar es Salaam.
2. Mwansoko, H.J.M (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI – Dar es Salaam.
3. Kihore. Y.M na Wenzake (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.
4. Massamba, D.P.B na Wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.
5. Saluhaya, M.C (2010) *Nadharia ya Lugha Kidato cha 5 & 6.* S.T.C Publishers- Dar es Salaam.
6. Masebo.J.A & Nyangwine, N (2009) *Nadharia ya Lugha kidato cha 5 & 6 .* Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.

7. Masebo, J. A & Nyangwine, N. (2008) *Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 & 6*, Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.

8. *Shafi A. S. (1999), Vuta ni N'kuvute, Oxford University Press, Dar es Salaam*

9. *Tuwa, h. (2007), Mfadhili, Maxmilian, Dar es Salaam,Dar es Salaam*

10. Shaaban R. (1967), Kufikirika, *Oxford University Press, Dar es Salaam*

11. Mbunda M. (1990), Usiku Utakapokwisha, DUP, *Dar es Salaam*

12. Emmanuel M. (1995), Morani, DUP, *Dar es Salaam*

13. Penina M. (1982), Nguzo Mama, DUP, *Dar es Salaam*

14. Ibrahim H. (1988), Kwenye Ukingo wa Thim, *Oxford University Press, Dar es Salaam*

15. *Mohamed, S. (1990)*, Kivuli Kinaishi, *Oxford University Press , Dar es Salaam*

16. Mohamed S. K. (1988), Fungate ya Uhuru, DUP, *Dar es Salaam*

17. Haji G. H (1995), Kimbunga, TUKI, *Dar es Salaam*

18. Theobald M. (1985), Chungu Tamu, TPH, *Dar es Salaam*

**VI. VITABU VYA PHYSICS: -**

1. Mehta, R. and V. K Mehta (2009) *"Principles of Physics for Class XI*" New Delhi, S.Chand and Company Ltd.
2. Nelcon, M and P. Parker (1995) *"Advanced level Physics"* 07th Edition, London, Heinmann Educational books.
3. TIE (2019) "*Physics for Advanced Level Secondary Schools*, Form Five, Dar es salaam, TIE.

**VII. VITABU VYA BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. T.I.E ;(2019), Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools Studenrs Books Form Five and Six.Tanzania Instute Education, Dar es Salaam
2. Mathematics, For Class XI, Volume I, S. CHAND
3. Mathematics, For Class XI, Volume II, S. CHAND
4. Mathematics, For Class XII, Volume I, S. CHAND
5. Mathematics, For Class XII, Volume ii, S. CHAND

**VIII. VITABU VYA JIOGRAFIA: -**


1. Pritchard J.M. (1979*) "Africa a study Geography for Advanced students"* London, Longman.

2. Msabila D. T (2003) *"Success in Geography climatology and Soil Science",* Dar es salaam, Afroplus Industries L.T.D

3. Prichard J.M. (1990) *"Practical Geography for Africa"* Longman.

4.Kamili, 2, *Physical Geography for Africa*, Dar es salaam, Afroplus Industries.

5. Msabila D.T. *Physical Geography*, Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.
6. Msabila D.T. (2006) *Human and economic Geography* (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.


IX. **VITABU VYA SOMO LA KIINGEREZA**


1. Ndambo,G.S & Kinunda, J.E. (2017). *Advanced Level English Language 1*, Form 5&6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
2. Kadeghe, M. (2010), *The Real English Textbook for Advanced Level,* Form Five, Dar es salaam, Jamana Printers Limited.
3. Kadeghe, M. (2010) *The Real English Textbook for Advanced Level,* Form Six. Dar es salaam, Jamana Printers Limited.
4. Asheli, N. (217) *Advanced Level English Language Structure & Stylistics*, Dar es salaam, APE publishers Ltd.
5. Lyi Kwei Armal, *the beautiful one are not yet born.*
6. Chunua Achebe, *A man of the people*
7. Heinrich Ibsen, *An Enemy of the people*
8. Ngungi wa Thiongo, *I will merry when I*


**XII. GENERAL STUDIES: -**


1. Bigirwamungu, J & Deogratias M.5th Edition (2019) *Understanding Advanced Level General Studies,* Dar es salaam, Mikumi Publishers.
2. T. I. E, 2010), *General Studies for Secondary Education*, Dar es Salaam, T.I.E